



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA**



Septemba 01, 2022

TAARIFA KWA UMMA

**MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA NDG.
SUNDAY DEOGRATIAS ANAWAKUMBUSHA WAZAZI NA WALEZI WOTE KUWAPA
WATOTO CHANJO YA MATONE YA POLIO**

Kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa POLIO nchini Malawi, Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa imeanza zoezi la kampeni ya utoaji wa chanjo ya matone ya kuzuia ugonjwa wa kupooza kwa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano (5).

Chanjo imeanza kutolewa leo tarehe 01 hadi tarehe 04 Septemba 2022, saa 1:30 asubuhi katika vituo vyote vya kutolea huduma za Afya, pia timu ya watalamu na wahamasishaji watapita nyumba kwa nyumba kwa lengo la kuhamasisha watoto wote wenye umri chini ya miaka mitano (5) wapate chanjo.

Aidha katika kampeni hii watoto wote ambao walichanja na wale ambao hawakuchanja chanjo ya matone ya POLIO watapatiwa chanjo ili kuwakinga na mlipuko wa POLIO ulio tangazwa nchini Malawi.

Chanjo ya matone ya POLIO inasaidia kuimarisha kinga ya mtoto dhidi ya maambukizi na madhara ya ugonjwa wa POLIO ambao ni ulemavu wa viungo na vifo kwa watoto. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, anatoa wito kwa wazazi/walezi wenye watoto chini ya umri wa miaka mitano (5) wahakikishe wanawafikisha watoto hao kwenye vituo vya afya vya Wilaya ya Ludewa ili wapatiwe chanjo ya POLIO.

**Chrispin B. Kalinga
Afisa Habari na Mawasiliano Serikalini
Halmashauri (W) Ludewa.**